


Nipashe Pg 9.
Ijumaa June 12, 2020

# Madereva, makondakta wa daladala washukiwa

**Na Mwandishi Wetu, *TANGA***
0715086344 WhatsApp / SMS

BAADHI ya Wakazi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga, wamewalalamikia madereva na makondakta wa daladala kwa kukatisha safari na kukaidi kuwashusha kwenye vituo kwa kisingizio cha kupanda kwa bei ya mafuta na ubovu wa barabara.

Wakizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki iliyopita, wakazi hao walidai kuwa vitendo hivyo vinazidi kukithiri kwa baadhi ya daladala zinazofanya safari kati ya kituo cha mjini kwenda maeneo ya Donge, Kichangani, Masiwani na Kange Kasera.

Walidai vitendo hivyo vilianza baada ya mvua kubwa kunyesha hivi karibuni kwa kisingizio cha ubovu wa baadhi ya barabara na kusababisha magari kuharibika.

"Wanachofanya hakiridhishi kabisa, sisi tumekubali kuongezewa nauli lakini badala ushushwe kwenye kituo chako unashusha mbali na hapo, hatujui tumfuate nani wa kukemea hili", alidai Aisha Hamdani, Mkazi wa Magomeni.

Zuberi Bashiru alidai kuwa: "Wanachofanya wao ni kujipangia cha kufanya, lakini pia baadhi yao wamekuwa na kugha mbaya bila kujua anayemjibu ni mtu wa rika gani, tunaomba mamlaka.husika ichukue hatua,

"Utakuta mama ana mtoto mdogo, anashuswa mahali ambapo itamlazimu tena kupanda bodaboda imfikishe anapoenda wakati angeshushwa kituo anapostahili gharama zisizo na lazima zisingekuwepo, hili jambo linatuumiza sana ukizingatia kila kukicha maisha yanapanda."

Baadhi ya madereva na makondakta, walisema sababu kupandisha nauli, kubadilisha njia kunatokana na baadhi ya barabara kuharibiwa mvua na kuharibu magari kwa kukwama kwenye madimbwi.

Kaimu Ofisa Mfawidhi wa Wakala wa Udhibiti wa Usafiri Nchi Kavu (LATRA), Mkoa wa Tanga, Michael Kimia amewaonya madereva na makondakta kuwa watachukuliwa hatua kwa kukiuka sheria na kanuni barabarani.

Kimia, alisema wanafanya kaguzi kila siku kudhibiti vitendo hivyo na vingine vya uvunjaji wa sheria kwa manufaa ya wananchi.